

Muhtasari


- Hali ya unyenyevu wa udongo unatarajiwa kuendelea kuongezeka kwa baadhi ya maeneo pwani ya kaskazini na kusini kutokana na mvua zinazoendelea.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili kuongeza uzalishaji wenye tija kutokana na mvua zinazotaraiwa

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hali ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika. Hali hi ilisababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kupanda kuelekea kaskazini mwa dunia na kuwepo katika nchi yetu hususani maeneo ya ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi liliendelea na kupelekea upepo wenye unyenyevu kuvuma kutoka kusini Mashariki. Joto la bahari la chini kidogo ya wastani liliendelea katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ya mifumo ilipelekea kuimarika kwa mifumo ya mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususani katika ukanda wa ziwa Viktoria.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2019

Kwa kipindi hiki mifumo ya hali ya hewa imepelekea mvua nyingi katika maeneo ya pwani ya kaskazini vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba. Kiasi cha mvua cha kati ya mm 200 mpaka mm 250 kimepatikana katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro na ukanda wa pwani ikiwemo Zanzibar. Maeneo mengine ya nchi hususani nyanda za juu kaskazini mashariki, kanda ya kati, magharibi, kusini na nyanda za juu kusini magharibi yamepata kiasi cha mvua za chini ya mm 26 kama inavyojieleza kwenye Kielelezo.



Kielelezo : Kiasi cha mvua katika kipindi cha Mei 11- 20, 2019.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2019

Katika kipindi hiki zao la mahindi kwa maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka lilikuwa katika hali nzuri kutokana na mvua za msimu zinazoendelea. Hata hivyo zao la mahindi limeathirika katika maeneo ya mkoa ya Dodoma, Singida na Tabora kutokana na vipindi vya ukavu vilivyojitokeza wakati wa msimu. Kwa upande unaopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususani baadhi ya maeneo ya Kilimanjaro, Moshi, Same na Kiteto hali ya upungufu wa wa mvua iliendelea kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao. Mazao ya mahindi na maharage kwa mkoa wa Kagera yanaendela vizuri. Wakulima kwa maeneo haya waliendelea na palizi na kuweka mbolea .Upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo yaliendelea kuwa katika hali nzuri kwa maeneo mengi ya nchi.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mitiririko ya maji kwenye mito kwa maeneo yaliyoendelea kupata mvua kiliendelea kuongezeka kutokana na mvua zilizoendelea kunyesha.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 21-31, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda wa mvua kupanda kuelekea kaskazini mwa dunia na kuwepo katika nchi yetu hususan maeneo ya ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuendelea na kupelekea upepo wenye unyevunyevu kuelekea pwani. Pia joto la bahari la juu ya wastani la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuendelea, hali hii inatarajiwa kusababisha migandamizo midogo ya hewa. Upepo katika levo ya 850mb inatarajiwa kuvuma kutoka mashariki kwa pwani yote na kutoka magharibi kwa maeneo yanayozunguka, hali hii inatarajiwa kuleta unyevunyevu zaidi baharini na hivyo kusababisha mvua. Joto la bahari la chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ya mifumo inaweza kupelekea kuimarika kwa mifumo ya mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususan katika ukanda wa ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MEI 21-31, 2019

Maeneo ya Kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

Maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki, pwani ya kaskazini, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Pwani na visiwa vya Unguja na Pemba, nyanda za juu kusini magharibi, pwani ya kusini, na kanda ya kusini yanatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache.

Maeneo ya magharibi mwa nchi yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

Maeneo ya kanda ya kati (Dodoma na Singida) yanatarajiwa kuwa na hali ukavu.

MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MEI 21-31, 2019

Hali ya mvua inayotarajiwa kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki, nyanda za juu kusini magharibi, pwani ya kaskazini na kusini, magharibi na kusini itaongeza hali ya unyevunyevu wa udongo na kusaidia ukuaji wa mazao. Ingawaje kwa upande wa maeneo ya mabondeni ya pwani ya kaskazini na mkoa wa morogoro hali ya unyevunyevu wa udongo unatarajiwa kuendelea kuongezeka hadi juu ya kiwango. Hata hivyo, mvua zinazoendelea kunyesha nchini hazitegemewi kuendelea kwa kipindi kirefu hususan maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki yataendelea kupata mvua kwa mwezi Mei 2019. Wakulima na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili kunufaika na mvua zinazotabiriwa kwa kipindi hiki.

HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA MEI 21-31, 2019

Hina cha maji kwenye mabwawa na mitiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu na kuvuna maji ya mvua pale inapowezekana kwa ajili ya matumizi ya baadaye.